JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA

BARAZA LA FAMASI

UHUISHAJI WA TAARIFA ZA WANATAALUMA WALIOPO KWENYE REJESTA KWA MWAKA 2025 NA UPATIKANAJI WA LESENI ZA UTENDAJI KAZI KWA MFUMO WA KIELEKTRONIKI

UTANGULIZI

1. DHUMUNI: Kutekeleza takwa la Vifungu Na. 22, 26 na 30 vya Sheria ya Famasi, Sura 311 (The Pharmacy Act, Cap 311).
2. WAHUSIKA: Wafamasia, Fundi Dawa Sanifu na Fundi Dawa Wasaidizi.
3. MFUMO WA UHUISHAJI: Mfumo wa Kielektroniki utakaomtaka mwanataaluma kuwasilisha taarifa zake za sasa katika Ofisi ya Msajili kwa mujibu wa Sheria na kudurufu (printing) leseni ya utendaji kupitia mfumo wa kielektroniki.

LENGO LA UTARATIBU

1. BARAZA:
   - Kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa wanataaluma
   - Kupata taarifa za mwanataaluma kwa wakati
2. WANATAALUMA:
   - Kupunguza gharama na muda wa ufuatiliaji wa leseni za utendaji
   - Kuongeza ufanisi wa taarifa za mwanataaluma
   - Kutoa taarifa za kitaalamu kwa wakati kila inapobidi.

UTARATIBU WA KUHUISHA TAARIFA ZA MWANATAALUMA KWENYE REJESTA

a) **FOMU:** Jaza fomu inayopatikana kwenye tovuti www.pc.go.tz kisha bonyeza huduma za kimtandao (Online Services Menu) kisha bonyeza Retention Application;

   a) Sign up: Kwa mwanataaluma ambaye hajawahi jisajili kwenye mfumo, *https://mis.pc.go.tz/pcmis.data/view/modules/registration/pharmacist-signup.php:*
   Kwa mwanataaluma mwenye akaunti, tumia nywila uliyotumia kipindi kilichopita: *https://mis.pc.go.tz/pcmis.data/*

b) **ADA:** Utapaswa kulipa ada ya kuhuisha usajili kwa mujibu wa Kanuni za Usajili wa Wanataaluma ya mwaka 2005 na Kanuni za Ada na Tozo ya mwaka kama ifuatavyo:-

Mfamasia	TZS 165,000/-
Fundi dawa sanifu	TZS 66,000/-
Fundi dawa msaidizi	TZS 44,000/-

b) **MUDA WA MALIPO:** Mwisho wa kulipia ada ni tarehe 31/12/2024, baada ya hapo utalazimika kulipa faini ya asilimia ishirini na tano (25%) ya kiwango ulichotakiwa kulipia.

MAMBO YA KUZINGATIWA WAKATI WA KUHUISHA TAARIFA ZAKO KWENYE REJESTA

a) JINA: Kama lilivyoainishwa katika cheti cha usajli kilichotolewa na Baraza (Registration, Enrollment, or Enlisting Certificate);

b) NAMBA YA USAJILI: (Registration, Enrollment or Enlisting Number): Personal Identification Number (PIN) kwa mifano ifuatayo:-

S/N	KADA	NAMBA YA USAJILI	KEY CODE	PIN (PERSONAL IDENTIFICATION NUMBER)
1.	Mfamasia	754	01	0000000 mfano 0100754
2.	Fundi Dawa Sanifu	1010	04	0000000 mfano 0401010
3.	Fundi Dawa Msaidizi	24	05	0000000 mfano 0500024

c) PICHA (Kwa mwanataaluma ambaye hajawahi kuhuisha leseni): Nakala laini ya picha ya uso (upload passport size photo) yenye Background ya bluu. Zingatia vipimo upana *350px* urefu *350px* kama mfano ufuatao;

d) MAFUNZO ENDELEVU

(Continuing Professional Development – CPD, Additional Qualification-Mfn. Masters, PHD, Professor, Other continuing Education - CE): Wasilisha nakala laini ya vyeti vya mafunzo endelevu aidha kozi za muda mrefu au muda mfupi; Pia kamilisha hatua za kuhuisha kwa kusoma kitita cha mafunzo na kujibu maswali kupitia kiunganishi katika akaunti yako.

e) LESENI YA UTENDAJI KAZI:

I. Baraza limeandaa utaratibu mpya wa uandaaji na uchapishaji wa leseni za utendaji kazi, ambazo kwasasa zitatolewa kwenye mfumo wa kielektroniki wa Baraza kupitia akaunti uliyoitumia kufanya maombi ya kuhuisha taarifa kwenye rejesta.

II. Kukamilisha maombi ya kuhuisha taarifa kwenye rejista, sasa utaweza kudurufu (printing) leseni yako ya utendaji wa taaluma.

Mfano wa leseni ya utendaji wa taaluma:



THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

PHARMACY COUNCIL

LICENSE TO PRACTICE

The Pharmacy Act

(Made under Sect.22 of The Pharmacy Act No. 1 of 2011)

I Hereby Certify that

JULIUS J NDYAKALIKA

PIN NO: XXXXXXX

Having complied with the provision of Section 22 of The Pharmacy Act, Cap 311 is entitled to practice as a **Full Registered Pharmacist** upon the terms and subject to the conditions set forth in the aforesaid Act and its Regulations thereto.

Issued:**30 July 2018** Expires on:**31 December 2022**

Registrar
Pharmacy Council

f) MALIPO:

(i) Control Number itapatikana moja kwa moja kwenye mfumo (*automatically*) wakati wa kuwasilishwa maombi sehemu ya Bill Creation na kutumwa kwenye namba yako ya simu.

(ii) Control Number hii itakuwa na uhai ambao utakoma matumizi tarehe 31/12/2024.

(iii) Tembelea akaunti yako sehemu ya Bill Creation kuweza kupata namba mpya ya malipo endapo utafanya malipo baada ya tarehe 31/12/2024 ambayo itaambatana na faini ya 25%:

g) USER MANUAL:

Kama unafanya maombi haya kwenye mtandao kwa mara ya kwanza, kabla ya kuanza kujaza taarifa zako kwenye *Pharmacy Council Online Retention Application System (PCORAS)* hakikisha unasoma *User Manual* ***https://www.pc.go.tz/files/PharmaceuticalPresonnelRetentionUserManual.pdf (pc.go.tz)***